# Ubabedume katika Ushairi wa Kiswahili: Mfano wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*

*John M. Kobia* na *Rose Mung'ahu*

## Ikisiri

Suala la uana limepewa kipaumbele miongoni mwa masuala yanayotafitiwa katika taaluma mbalimbali zinazohusu maisha ya binadamu. Majukumu ya jinsi ya kike na jinsi ya kiume ni suala ambalo linaendelea kuzua mgogoro miongoni mwa watu wa jamii mbalimbali. Hata hivyo, utafiti wa uana unaozingatia jinsi ya kiume katika Kiswahili, hususan fasihi simulizi haujashughulikiwa kwa kina. Tafiti nyingi zilizopo zimeshughulikia masuala ya kike. Kuna haja ya utafiti kufanywa kuhusu suala la jinsi ya kiume katika fasihi, hususan katika ushairi wa jadi wa Kiswahili. Makala haya yanachunguza suala la ubabedume katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwa kuzingatia majukumu, sifa na nafasi ya mwanamume katika utenzi huu. Makala yameongozwa wa nadharia ya ubabedume inayosisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume kwa kuzingatia jamii, maandishi na matukio au maelezo ya kihistoria.

## 1.0 Utangulizi

Madai ya Finnegan (1970:108 - 109) na Knappert (1983:54-56) kuwa tenzi za Kiafrika hazikumudu sifa zote za utenzi yaliwachochea watafiti wengi wa Kiafrika kama Okpewho (1979), Mbele (1986), na Mulokozi (1999) kufanya utafiti wa tenzi za Kiafrika. Matokeo ya uchunguzi wao yalikuwa vigezo vya kubainisha sifa za tenzi na hivyo kudhihirisha kwamba katika Afrika kuna tenzi, kinyume na madai ya awali ya Finnegan (1970) na Knappert (1983).

Mojawapo ya mifano ya tenzi katika Afrika ni *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Kama anavyodokeza Mulokozi (1999:9-10), *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni wa Kiafrika. Hii ni kutokana na sifa zinazouzingira utenzi huu pamoja na sifa zinazomzingira shujaa wa utenzi huu ambaye ni Fumo Liyongo. Baadhi ya sifa zinazouzingira utenzi huu ni: Kwanza, masimulizi ya kihadithi, ambapo hadithi inayosimuliwa ina ushikamano na utoshelezi. Pili, umetungwa kishairi ambapo unaimbika. Tatu, utenzi huu unahusu matukio muhimu ya kihistoria na kijamii. Nne, unasimulia kuhusu shujaa na ushujaa. Tano, umeathiriwa na muktadha wa utunzi na uwasilishaji. Sita, maudhui ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni baadhi ya yale yanayojitokeza katika tenzi nyingine za Kiafrika na kiulimwengu kwa jumla. Maudhui haya ni kama vile ushujaa, utawala, utetezi na usaliti. Kulingana na Mulokozi (1999:1) mtunzi wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni Muhamadi bin Abubakar bin Omari al-Bakari ambaye alijulikana zaidi kama Muhamadi Kijumwa. Kijumwa alipata hadithi ya Fumo Liyongo kutokana na mapokezi simulizi ya Waswahili wa mwambao mwa Kenya. Hakubuni hadithi hii bali alisimuliwa kisha akaihifadhi upya kwa maandishi katika umbo la utenzi.

*Utenzi wa Fumo Liyongo* unasimulia kisa cha Liyongo kinachohusu mgogoro kati ya Fumo Liyongo na binamu yake, mfalme wa Pate. Japo mfalme huyu hatajwi katika utenzi huu kwa jina, ametajwa katika mapokezi mengine kuwa Daudi Mringwari. Liyongo anadokezwa kama kijana barobaro mwenye sifa kwa nguvu na ushujaa wake. Aliishi eneo la Shaka, jimbo la Ozi, nyumbani kwake Ungwana wa Mshasha. Sifa za Liyongo zilienezwa kote Pate na Sultani Daudi, miongoni mwa Wapate ambao hawakuamini. Jambo hili lilimwelekeza Sultani kumpelekea Liyongo barua ya wito wa kuja Pate ili Wagala wamwone. Liyongo anapanga safari kwenda Pate ambayo ni safari ya siku nne lakini yeye anachukua siku mbili tu. Anapokaribia Pate mjini, anaipuliza panda yake kisha inapasuka; anapuliza ya pili na inapasuka pia. Anapopuliza ya tatu, anaingia mjini hadi barazani kwa Sultani. Watu wanakusanyika kumwona ambapo wanashuhudia akitua mzigo wake na kutoa vitu vya kutosha kujaza nyumba nzima. Jambo hili linawaelekeza kusadiki kwamba, Liyongo hakika ni mwenye nguvu. Wanamnasihi Sultani awaruhusu wapate mbegu yake, jambo ambalo Sultani anawakubalia. Liyongo anaozwa mke ambaye anamzalia mwana wa kiume. Sifa za Liyongo zinaenea zaidi huku Sultani akihofu na kueneza fitina. Anahofu kuwa Liyongo atamnyang'anya ufalme. Liyongo anapotambua kuwa mfalme ana njama ya kumuua, anatorokea nyikani na kuishi miongoni mwa Wasanye, Wadahalo, Waboni na Watwa. Mfalme anajaribu kuwashawishi Wadahalo na Wasanye wamuue Liyongo na kuwaahidi reale mia iwapo watamletea kichwa chake. Wasanye na Wadahalo wanafanya urafiki na Liyongo kwa njama. Wanashauri kuwa wawe wakila pamoja kikowa. Chakula wanachokila ni makoma ambayo wanayaangusha kutoka mtini kwa zamu. Zamu ya Liyongo inapofika wanataraji kwamba atakapopanda juu ya mti kuyaangua, watapata nafasi ya kumuua, kwa mishale yao akiwa juu ya mti. Kwa bahati, Liyongo anagundua hila hii kisha anaamua kuangua makoma kwa mishale yake akiwa chini.

Mulokozi (keshatajwa) anaendelea kutueleza kuwa, Wadahalo na Wasanye wanapompasha Sultani habari kuwa Liyongo hawezwi, anawaambia warudi porini na kumweleza Liyongo kuwa mjini hakuna hatari tena, kisha waambatane naye kuja mjini. Liyongo kwa kuwaamini anarudi nao mjini Pate. Baada ya siku chache, Sultani anaitisha ngoma ya 'gungu' na 'mwao' na kuwaalika mashaha wote wa ngoma, miongoni mwao akiwa Liyongo. Askari wanamzunguka na kumshika wakati wa ngoma na kumtia gerezeni na kuamua auawe. Liyongo anaambiwa afanye ombi lake la mwisho wakati wa kuuawa kwake. Anaomba achezewe ngoma ya 'gungu' na 'mwao'. Ngoma inapoanza, anampelekea mama yake ujumbe kupitia kwa kijakazi Saada. Anamtaka mamake ampikie mkate wa wishwa na kati yake aweke tupa ya kukerezea vyuma. Saada anapofika gerezani, askari wanamnyang`anya mikate mizuri na kuuacha ule wa wishwa apelekewe

Liyongo. Mara tu ngoma inapoanza na kunoga, Liyongo anatoa ile tupa na kukata minyororo na kuvunja lango la gereza kisha anatoroka na kurejea nyikani.

Baada ya Sultani kushindwa jaribio hilo, anamshawishi mwanawe Liyongo amwendee babake na kumhadaa afichue siri ya nguvu zake. Sultani anamwahidi mwana wa Liyongo kuwa atamwoza bintiye pamoja na kumpa uwaziri iwapo atafaulu. Liyongo anapoendewa na mwanaye, anatambua kuwa mwanaye ametumwa na adui. Hata hivyo hasiti kumfichulia siri ya nguvu zake. Anamfichulia kuwa kinachoweza kumuua ni sindano ya shaba ya kitovuni tu! Sultani anapopata habari hii anafurahi na kumlimbikizia mwanae Liyongo zawadi nyingi. Anampa sindano ya shaba na kumtaka arudi tena Shaka na kumuua babake. Mwanae Liyongo anarudi kwa babake na kusubiri hadi anapokuwa amelala kisha anamchoma sindano ya shaba kitovuni. Liyongo anatoka usingizini kwa ghadhabu, anachukua upinde na mshale wake na kuelekea kisimani ambako anapiga goti na kutia mshale katika upinde akiwa ameuelekeza mjini kisha anaaga. Watu wajapo kisimani na kumuona, wanadhani angali hai na kwa siku tatu mfululizo hawaendi kisimani kuteka maji kwa woga. Mamake anachukua nasaha ya watu na kuamkia kila siku kumbembeleza Liyongo kwa mashairi ili aondoke ndipo sasa watu waweze kuteka maji. Anafanya hivyo bila mafanikio. Maiti ya Liyongo inaoza na kuanguka ndipo watu wanatambua kuwa amekufa.

Habari za kifo cha Liyongo zinamfurahisha mfalme ambaye anamweleza mwanaye Liyongo kuhusu kifo cha babake. Mwanawe Liyongo kinyume na matarajio anacheka, jambo ambalo linamfanya mfalme kumnyang'anya kila alichokuwa amempa na kumfukuzia mbali. Anakimbilia porini kwa Wagala anakofia.

Muhamadi Kijumwa alipata taarifa za Fumo Liyongo kutokana na fasihi simulizi ambayo ilijumuisha tendi simulizi na nyimbo za Waswahili. Maelezo anayotoa Kijumwa ni muhtasari wa yale yanayomhusu Liyongo; huenda usimulizi wake haudokezi kikamilifu yote yaliyomhusu Liyongo hasa yale yanayopatikana katika nyimbo zake. Hivyo basi, *Utenzi wa Fumo Liyongo* ulioandikwa na Kijumwa ni mojawapo ya simulizi zinazomhusu Liyongo kama vile simulizi ya Steer (1870:438). *Utenzi wa Fumo Liyongo* uliimbwa na hata ungali unaimbwa katika sherehe za Waswahili.

Madhumuni ya makala haya ni mawili; kwanza, kufafanua jinsi ubabedume unavyojitokeza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Pili, kupambanua mchango wa utamaduni wa Waswahili katika kukuza ubabedume katika *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

**2.0 Uhakiki wa Maandishi Yamhusuyo Liyongo**

Maoni na mitazamo tofauti kutoka kwa wasomi mbalimbali yametolewa kuhusu *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwa jumla. Mbele (1997:7-14) alitambua kuwa maoni mbalimbali yametolewa kuhusu *Utenzi wa Fumo Liyongo* na kuchapishwa ambapo uhakiki wa awali ulielekea kuwa wa jumla bila kujaribu kuzama katika uchunguzi wa kipengele maalumu katika utenzi huu. Utafiti huu umechunguza kipengele maalumu cha usawiri wa mwanamume katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwa kuzingatia sifa na majukumu anayotengewa mwanamume katika jamii ya Waswahili.

Ili kuelewa maudhui ya utenzi huu ni muhimu kuwe na ufahamu wa kiini chake kwa misingi ya utamaduni, historia na maandishi. King'ei (2001) anasema kuwa *Utenzi wa Fumo Liyongo* unaweza kuchunguzwa kwa kuzingatia mtazamo wa kiethnolojia ambao huchukua fasihi kama kiwakilishi cha jamii ya mwanadamu na thamani zake za kitamaduni, mielekeo na desturi zake. Anasema kwamba wahusika katika fasihi kama vile Fumo Liyongo ni umbuji wa utamaduni ambapo ni kielelezo cha wenyeji wa kiasili wa jamii ya Waswahili wa Mwambao mwa Kaskazini, Kenya. Utafiti huu umechunguza jamii ya jadi ya Waswahili na kuchanganua nafasi na majukumu anayopewa mwanamume kwa misingi ya utamaduni, itikadi na desturi za jamii ya Waswahili. *Utenzi wa Fumo Liyongo* umekuwa kigezo mwafaka cha kuchunguzia hali hii.

Jamii nyingi za Kiafrika humtukuza mwanamume kupitia mila, desturi na itikadi zao. Momanyi (2007:12-32) anaeleza kuwa katika jamii ya Waswahili kuna itikadi zinazohalalisha mamlaka ya mwanamume kwa misingi ya desturi za kitamaduni, itikadi za kidini na tofauti za kijinsia. Tangu jadi wanaume katika jamii hii wamekuwa watawala wa kitamaduni wa mfumo wa ishara za ubwana ambapo lugha hutumiwa kufafanua ujinsia. Ujinsia unafafanuliwa kama pande mbili tofauti na kinzani ambazo hubainisha tofauti kati ya wanaume na wanawake. Tofauti hizi huendelezwa kijamii na kitamaduni. Mfano huu wa ubwana unaohusisha imani za kijumla za kijamii kuhusu tofauti za kijinsia umeundwa na mwanamume. Kuna haja ya kuchunguza vijenzi vya ujinsia kwa kuzingatia jinsi ya kiume, ili kubainisha namna baadhi ya vijenzi hivi vinavyomtazama mwanamume. Utafiti huu umechunguza ushairi wa Kiswahili katika jamii ya Waswahili. Uhakiki wa vijenzi vya jinsi ya kiume ulifanywa kwa kuzingatia asili yake na athari yake kwa mwanamume katika jamii ya sasa ya Waswahili. Uhakiki wa ushairi ulifanywa katika jamii ya Waswahili kwa kuzingatia usawiri wa mwanamume katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

Itikadi ni dhana ambayo haiwezi kutenganishwa na ubabedume. Coward na Ellis (1977:71) wanasema kuwa itikadi ni mfumo changamano na wenye ukinzani wa ishara kama usemi, taswira na visasili ambavyo kwavyo tunajihisi katika

mahusiano na wengine katika jamii tunamoishi. Kuna itikadi za kuumeni ambazo zinamkuza na kumtawaza mwanamume katika jamii ya Waswahili. Itikadi hizi huwasilishwa kupitia kwa baadhi ya tenzi. Zinafaa kuchunguzwa upya kulingana na ulimwengu wa sasa wenye mabadiliko na utandawazi. Utafiti wetu umechunguza maudhui ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* na kutathmini nafasi ya maudhui haya katika ulimwengu wa sasa. Utafiti ulizingatia majukumu na nafasi aliyotengewa mwanamume katika jamii ya Waswahili kisha ukahakiki athari zake kwa mwanamume katika jamii ya sasa ya Waswahili.

Jeftha (2006) amefanya utafiti kuhusu vijenzi vya ubabedume na tabia ya kuthubutu mambo miongoni mwa vijana chipukizi. Matokeo ya utafiti wake ni kwamba, mwelekeo na mtazamo wa kiitikadi na kitamaduni kuhusu mwanamume umekuwa na athari kubwa kwa tabia za kila siku za vijana chipukizi kuelekezwa kwa maisha yao ya kila siku. Utafiti wetu umechunguza mchango na athari za itikadi na tamaduni za kiasili kwa tabia na hulka za kila siku anazokuwa nazo mwanamume.

**3.0 Nadharia ya Utafiti**

Makala haya yanatumia nadharia ya ubabedume. Nadharia ya ubabedume inajikita katika maumbo ya vitambulishi vya jinsi ya kiume kwa kuzingatia jamii, maandishi na matukio au maelezo ya kihistoria (Wells na Holland, 2001:16). Utafiti huu umezingatia mkondo wa nadharia ya ubabedume unaowania kuhalalisha desturi za jinsia ya kiume na ubabedume. Kulingana na Wells na Holland (2001:2), mwasisi wa nadharia hii ni Robert Bly wa Marekani. Nadharia hii ilitokana na mwamko wa vuguvugu la wanaume ambalo lilichochewa na kazi za Robert Bly na wengine (Chafetz, 1974). Kichocheo cha vuguvugu la wanaume kilitokana na uhakiki wa jinsi ya kiume na utawala wa wanamume unaoathiri kila sehemu ya jinsi ya kike pamoja na mageuzi ya miaka ya 1960. Huu ulikuwa wakati wa upeo wa mgogoro wa itikadi za kijamii katika nchi za Marekani ambazo zilihitaji kuzingatia upya majukumu ya kijinsia. Mgogoro huu ulihusu nafasi na majukumu ya kijinsia katika jamii.

Mihimili ya nadharia ya ubabedume ifuatayo ilitumiwa katika utafiti huu kuhakiki nafasi ya mwanamume katika jamii, majukumu yake na hulka anayotakiwa kuwa nayo katika jamii: Kwanza, utawala wa mwanamume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume kwa misingi ya jamii, maandishi, matukio na maelezo ya kihistoria (Wells na Holland, 2001). Pili, wanaume wametawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za rasilimali zenye thamani katika jamii kama vile kazi, pesa na taasisi za kijamii zenye nguvu kama vile serikali na dini (Collins, 1971 na Sokoloff, 1980). Tatu, desturi za jinsi ya

kiume zimehalalishwa kwa madai kwamba wanaume wengi husukumwa kutenda kulingana na ubabedume (Jeftha, 2006). Lazima mwanamume awe mshindi katika hali zinazohitaji nguvu za kimwili, awe na uwezo wa kuamua na kufikiri kiurazini.

Mhimili wa nne wa nadharia ya ubabedume unasisitiza kuwa kutokana na mabadiliko na changamano katika jamii, mgawanyo wa majukumu ya kijinsia ya kitamaduni hauna nafasi katika ulimwengu wa sasa. Ulifaa nyakati za awali (Bliss, 1974; Marwel, 1975; na Peplau, 1983). Tano, wanaume wameweka utambulisho wao katika sura na mfano wa Mungu wa kiume kwa manufaa yao wakizingatia kwamba mwanamume alipewa mwanamke kama mwenzi kutoka kwa ”Mungu wa kiume” (Ruether, 1974:156). Sita, wasiwasi unaowakumba wanaume kwa kupoteza heshima na ubainifu wa majukumu yao ni halali (Nayak na Kehily, 2008 na Fave, 1986a, 1986b,1980). Mwisho, maeneo ya ubabedume yanajitokeza katika desturi kwa jumla kupitia maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi na kukidhia familia, kuwa na tajiriba na shari ya kijinsia, ukakamavu, urazini, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani na kuthubutu mambo (Chafetz, 1974 na Doyle, 1985).

## 4.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti ulifanywa kwa njia kuu mbili: utafiti wa maktabani na nyanjani. Dodoso lilitumiwa ili kupata habari zinazohusiana na suala la utafiti. Tulisoma na kuhakiki *Utenzi wa Fumo Liyongo* ili kuchunguza kwa kina suala la usawiri wa mwanamume katika ushairi wa Kiswahili. *Utenzi wa Fumo Liyongo* ulihakikiwa kwa kuainisha nafasi, sifa na majukumu aliyotengewa mwanamume katika jamii ya Waswahili. Pia, tulibainisha namna tamaduni na itikadi za jadi zilivyochangia hulka ya mwanamume katika jamii ya Waswahili.

Utafiti wa maktabani ulijumuisha kutembelea maktaba na makavazi mbalimbali kama vile, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Chuo Kikuu cha Moi, Chuo Kikuu cha Maseno, Maktaba Kuu ya Lamu, Makavazi Kuu ya Lamu, ‘Fort Jesus Resource Centre’, na ‘Swahili Cultural Research Centre’- Mombasa ili kupata maandishi na habari kuhusu Waswahili na fasihi simulizi ya Waswahili. Pia, iliwezekana kupata maandishi kuhusu *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Utafiti wa nyanjani ulitekelezwa kwa kuzuru Wilaya za Lamu na Tana River ambayo ni maeneo ya Waswahili na aliyoishi mtunzi wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Utafiti wa nyanjani ulisaidia kuchunguza mahali Fumo Liyongo alikoishi, alikofia na alikozikwa. Pia, habari kamili na halisi kuhusu jamii ya Waswahili zilipatikana. Tulizuru eneo la Tossi Kipini ambako ndiko alikofia na kuzikwa Fumo Liyongo. Tuliweza kupata habari za Kilindini kuhusu Fumo Liyongo kama vile kisimani alipofia, gofu la

iliyokuwa ofisi yake na mahali alikozikwa. Pia, tuliweza kupata itikadi za wenyeji kumhusu Fumo Liyongo.

Tulitembelea 'Swahili Cultural Research Centre - Mombasa' kumhoji Sheikh Nabhany ambaye alitudokeza mengi kuhusu jamii ya Waswahili, mila na desturi zao na athari za elimu na maisha ya sasa kwa jamii ya Waswahili. Sheikh Nabhany ni mtaalamu wa mila, desturi, itikadi na historia ya Waswahili. Alitupa habari muhimu kuhusu Fumo Liyongo.

Kupitia njia ya kutangamana na kuwasaili Waswahili wenyeji wa Lamu na Tana River, tuliweza kuchunguza na kufahamu zaidi misingi ya kihistoria na kitamaduni ambayo utunzi wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* umejikita. Tuliweza pia kupata ufahamu kuhusu tabia, mielekeo, mila na desturi za Waswahili; itikadi zao na mtazamo wao kuhusu nafasi ya mwanamume katika jamii na katika ndoa. Athari zake katika jamii ya sasa zilichanganuliwa na kuhakikiwa. Habari tulizopata zilichangia kukuza na kuimarisha suala la utafiti kuhusu usawiri wa mwanamume katika jamii ya Waswahili.

Watu 12 walihojiwa. Idadi hiyo inajumuisha vijana kwa wazee wenye umri kati ya miaka 25 na 85, ambao walijumuisha wanawake 5 na wanamume 7. Kwa kuzingatia umri huu, tuliweza kupata habari kama vile mtazamo wa vijana na wazee kuhusu mila na desturi za Waswahili. Hili lilitekelezwa katika viwango mbalimbali kama vile, ndoa za kijadi, nafasi na majukumu ya mume na mke katika ndoa, namna maisha ya sasa yalivyoathiri mila na desturi za kijadi za Waswahili na maisha yao kwa jumla. Hili lilifanywa hasa kuhusiana na nafasi ya mwanamume katika jamii, na ndoa. Pia, tuliweza kufahamu mtazamo wa wanawake na wanaume kuhusu ndoa, nafasi na majukumu yao katika ndoa, mchango na athari za dini katika kuimarisha ndoa, mchango na athari za itikadi, mila na desturi katika kuimarisha na kuhifadhi hadhi, utukufu na nafasi ya mwanamume katika jamii ya Waswahili.

Pia, tuliweza kupata fursa ya kutangamana na wenyeji kupitia kuhudhuria harusi zao, kuzuru majumbani na kazini kwao na kuhudhuria mahakama za kadhi. Hili lilituwezesha kupata habari na hali halisi kuhusu maisha yao halisi ya kila siku, mila, desturi na itikadi zao.

**5.0 Uchanganuzi wa Data**

Juhudi za kupata taswira ya mwanamume katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* zimemlenga Fumo Liyongo. Usawiri wa mwanamume umedhihirisha ubabedume ambapo umejikita katika fasihi ya Kiswahili. Ubadedume umejitokeza kupitia kwa taswira zifuatazo:

**5.1 Mwanamume ni Mwenye Nguvu na Shujaa**

Fumo Liyongo amedokezwa kama mwenye nguvu na ushujaa. Sifa hizi zinabainika mara tu anapobalehe kama tunavyoelezwa kupitia ubeti ufuatao:

6. Liyongo kitakamali
akabalighi rijali
akawa mtu wa kweli
na haiba kaongeya

Sifa ya ushujaa inajitokeza kupitia katika matukio mbalimbali maishani mwa Liyongo. Anabainisha nguvu zake za kimwili anapochukua siku mbili kutembea safari ya mwendo ambao kawaida uliwachukua watu siku nne, kama inavyobainika kupitia beti hizi:

25. Na mtu kitoka Shaka
hata Pate ukafika
siku nne kwa haraka
alo hodari sikiya

26. Liyongo akikabili
ndiya kenenda rijali
alikwenda siku mbili
na ya pili ni kungiya

Pia, anatenda kitendo ambacho si cha kawaida kwa binadamu: anapasua panda mbili kwa kuzipuliza tu. Beti zifuatazo zinabainisha tukio hili.

27. Liyongo kenda muini
akipata mlangoni
panda katia kanwani
kivuzia kapasuwa

30. Liyongo asimuhuli
akaipija ya pili
pandaye isihimili
na ya pili kapasuwa

Aina ya panda aliyopuliza Liyongo imehifadhiwa katika makavazi ya Kitaifa ya Ngome ya Yesu, Mombasa. Inaitwa ‘Bungoma Buffalo Horn’. Ina maandishi: Nabahani: ‘Sultani yuaja kukutana nawe. Utawala wa watu ni wake’.

Liyongo anaubeba mzigo wenye uzani mzito usioweza kubebwa na binadamu wa kawaida, kulingana na ubeti ufuatao:

37. Kisa katiti kutuwa
mkobani akatowa
zitu alizotukuwa
nyumba ndima nisikiya

Liyongo ni shujaa wa vita anayelinganishwa na simba; jambo ambalo linabainisha nguvu zake za vita. Anapolinganishwa na simba, inabainisha nguvu na ushupavu wake vitani. Angekumbana na watu wengi na wasiweze kumkabili bali kutorokea mbali; beti zifuatazo zinabainisha haya:

12. Mfalume kawambiya
Wagala kiwasifiya
'huwegema watu miya
wasiweze hukimbiya'

13. Ni mwanamume swahihi
kama simba una zihi
usiku na asubuhi
kutembea ni mamoya

Liyongo anaporejelewa kwa kutumia tashibihi ya simba, inabainisha ukamilifu wake kama mwanamume, kishujaa na kinguvu. Hii inaonesha urijali wake ambao ni sifa inayoambatanishwa na mwanamume katika jamii ya jadi ya Waswahili. Sifa ya ushujaa anayoimiliki Liyongo inakidhi mtazamo wa mhimili wa nadharia ya ubabedume inayoongoza utafiti huu. Hii ni kulingana na Chafetz (1974) na Doyle (1985) kwamba maeneo ya ubabedume yanajitokeza katika desturi kwa jumla kupitia maumbile na nguvu za kimwili. Tuliowahoji katika Mitaa ya Ozi, Kipini na Tossi Wilayani Tana River (Saada, Kefa, Hama, Bakari na Obo) walibaini kwamba Liyongo alikuwa shujaa aliyetegemewa na jamii ya Waswahili kwa ulinzi na utetezi dhidi ya maadui.

**5.2 Mwanamume kama Mbabe**

Liyongo amedokezwa kuwa mnene wa maumbile. Umbile lake lilikuwa kubwa la kutisha. Beti zifuatazo zinabainisha haya:

14. Ghafula kikutokeya
mkoyo hukupoteya
tapo likakuwiliya
ukatapa na kuliya

15. Mato kikukodoleya
ghafula utazimiya
kufa kutakurubiya
kwa khaufu kukungiya

Maumbile ya Liyongo yanakidhi matarajio ya jamii ya Waswahili kuhusu mwanamume ambaye hutarajiwa kuonesha na kudhihirisha ubabe. Hakika Liyongo ni mbabe wa kiwango cha juu hali ambayo Wagala wanapomshuhudia, wanajawa na hofu na kukiri kwamba hakika alikuwa mtu wa vita. Tunapata haya kupitia beti zifuatazo:

34. Nipate, akamwambiya
kipita akatokeya
Wagala wakashuhudiya
khaufu ziliwangiya

35. Ruhu zikenda kishindo
zimo zao hakoma ondo
huyo ni bwana wa kondo
ashindaye jeshi miya

Maumbile na ubabe wa Liyongo unaendelea kubainika tunapoambiwa kupitia ubeti ufuatao kuwa:

7. Kimo kawa mtukufu
mpana sana mrefu
majimboni yu maarufu
watu huya kwangaliya.

Umaarufu wa Liyongo ambao ulitokana na maumbile yake ulisababisha wengi kuja kumwona kwa shauku ya kutaka kumshuhudia. Ubabe wa kimwili wa Liyongo ulimpa ujasiri ambapo hakuogopa kitu au mtu yeyote. Nadharia inayoongoza utafiti huu imedokeza kupitia Chafetz (1974) na Doyle (1985) kwamba ubabedume unajitokeza katika desturi kwa jumla kupitia maumbile na nguvu za kimwili. Wahojiwa (Kefa, Hama, Bakari na Obo) wa Tana River walibainisha kuwa sifa za ubabe za Liyongo zilimpa sifa kuu miongoni mwa Waswahili.

Mwanamume amepewa sifa ya ubabe katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Sifa ya ubabe ndiyo inayompa umaarufu na kumwezesha kutekeleza baadhi ya majukumu anayokabidhiwa katika jamii ya Waswahili kama vile kuwa mlinzi, mtetezi na mkidhia jamii (wahojiwa Saada, Kefa, Salim, Hama, Bakari, Obo na Nabhany). Kulingana na hali ilivyo sasa mwanamume hahitaji nguvu za kimwili kubainisha umaarufu wake. Baadhi ya mambo aliyoyatenda ambayo yalihitaji nguvu za kimwili sasa yanafanywa kwa urahisi. Kuna uvumbuzi wa teknolojia ambao umezua uundaji wa mashine inayotenda kazi kwa urahisi pasipo kuhitaji nguvu nyingi za kimwili. Wahojiwa wetu waliona kuwa kinachompa mwanamume hadhi na utukufu katika jamii ni elimu na uwezo wa kiuchumi kuliko ubabe.

### 5.3 Mwanamume kama Rijali

Katika dhana na muktadha wa Kiafrika ubabe wa kimwili huambatana na urijali. Hivyo basi, Wagala wanapovutiwa na umbo la Liyongo, hawasiti kutaka kupata ‘mbegu’ yake. Hii inamaanisha kwamba Liyongo alikuwa mwanamume kikamilifu, mwenye nguvu na uwezo wa kiume; ndipo anatajwa kama mwanamume ‘sahihi’ na ‘rijali’. ‘Sahihi’ na ‘rijali’ yametumiwa kwa minajili ya tafsida kurejelea nguvu za kiume, kuambatana na miiko inayozingatia jamii ya Waswahili kuhusiana na nguvu za kiume. Inabainika kuwa Liyongo alikuwa kamilifu wa nguvu za kiume aliye na uwezo wa kujamiiana. Tunafahamu haya kupitia beti zifuatazo:

6. Liyongo kitakamali
akabalighi rijali
akawe mtu wa kweli
na haiba kaongeya.

13. Ni mwanamume sahihi
kama simba una zihi
usiku na asubuhi
kutembea ni mamoya.

Tafsida za mwanamume ‘sahihi’ na ‘rijali’ zimetumiwa kulingana na muktadha wa utambaji wa utenzi huu, ambao ni utamaduni wa Waswahili wa Pwani. Haikuruhusiwa kufafanua tafsida hizi ambazo zinarejelea uwezo wa kiume kwa uwazi zaidi. Hata hivyo, kupitia kwa tafsida hizi tunapata dhana ya ukamilifu wa Liyongo kama mwanamume kamili: mwenye uwezo wa kuendeleza kizazi kwa

kuwa alikuwa na nguvu na uwezo wa kiume. Katika jamii za Kiafrika, hasa jamii ya Waswahili, hali hii inabainisha ukamilifu wa mwanamume; hali ambayo ilimpa mwanamume hadhi na kumfanya kukubalika katika jamii. Nadharia ya ubabedume inayoongoza utafiti huu imedokeza kupitia Jeftha (2006) kwamba hali ya mwanamume kuonekana dhaifu ama asiye na ufanisi katika mambo ya kujamiiana ni tishio kubwa kwa taadhima ya mwanamume. Mtazamo na hali hii ndiyo inayomwelekeza Fumo Liyongo kuwa mwepesi wa kuchanga mbegu yake kwa Wagala ili kuthibitisha umaarufu wake wa kuwa na nguvu za kiume.

Nyakati za sasa, hii ni hali ambayo itamtia mwanamume aibu iwapo atajikuta katika hali ya kupata watoto bila kuwajibika katika ndoa. Ulimwengu wa sasa unazingatia upangaji wa uzazi na uwajibikaji kindoa. Isitoshe imani ya dini kama vile ya Kiislamu haimruhusu mtu kupata mtoto nje ya ndoa (mwanaharamu). Hivyo basi, kile kilichompa mwanamume umaarufu kiasili kwa kutajika kuwa "mwanamume sahihi" ndicho hicho ambacho kitamtia fedheha na kumweka katika hali tata katika ulimwengu wa sasa. Kama anavyosema mhojiwa wetu Jeftha, matendo ya ubabedume wa kiasili unaoambatana na kujamiiana bila kuwajibika imethibitishwa kuwa hatari na tatizi. Haya ni kulingana na hali ya sasa ya maambukizi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI.

Wanaume wameshurutika kutofanya mapenzi kiholela. Wanaelekezwa kuwa waaminifu katika ndoa na katika uhusiano wao wa kimapenzi. Wanaume wanaozingatia kubainisha na kudhihirisha kuwa 'wanaume kamili' kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanawake wengi wameambukizwa ugonjwa hatari wa UKIMWI na kuaga dunia. Haiwezekani kuwa mwepesi wa 'kuchanga mbegu' kiholela ili kutajika kuwa "mwanamume sahihi" kama anavyofanya Liyongo katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* pasipo kuhatarisha maisha.

Sifa anayoidokeza Liyongo inapatana na mihimili ya nadharia ya ubabedume inayoongoza utafiti huu. Kiasilia mwanamume anapenda sifa nzuri na utukufu ili apate kusifiwa na kutukuzwa, ama urijali, vipawa au fanaka zake. Chafetz (1974 :35-36) amebainisha haya kupitia nadharia ya ubabedume inayoongoza utafiti huu anaposema kuwa kiasilia, mwanamume hutaka kumiliki sifa za kuwa na tajiriba na shari ya kijinsia, ukakamavu, umantiki, urazini, uongozi, kutaka makuu na majivuno.

### 5.4 Mwanamume kama Mkimu Jamii

Kutokana na tukio la kikoa na makoma, Fumo Liyongo anapata usawiri wa kuwa mkimu jamii. Anajiunga na wanaume wenzake kukidhi hitaji la jamii la chakula. Wanashirikiana kutungua makoma kwa zamu. Katika beti zifuatazo

tunafahamishwa namna walivyounda kikoa ili kuhakikisha jukumu lao la kukidhia jamii linatekelezwa kwa utaratibu:

56. Siku moya wakanena
natuleni waungwana
kikowa ni tamu sana
karamu 'sotindikiya

58. Likisa shauri lao
wakenenda kwa kikao
mkoma waupatao
hupanda mtu mmoya

Haya yanaafikiana na nadharia ya ubabedume inayoongoza utafiti huu, ambapo mwanamume hutarajiwa kuweza kukimu familia. Doyle (1985:107) anadokeza kuwa mwanamume anapaswa kukimu familia kikamilifu kulingana na matakwa na matarajio ya jamii ya kiasili.

Wanakikoa walitaka kutumia tukio la kuunda kikoa kwa nia mbaya ya kupata nafasi ya kumdhulumu Liyongo kwa kunuia kumwangamiza. Imebainika wazi kwamba, Liyongo ametimiza matakwa na matarajio ya jamii kuwa mkimu wa jamii akiwa mwanamume. Kwa hivyo, katika jamii ya kitamaduni ambayo huzingatia mfumo wa kuumeni, Liyongo ana hadhi na haki ya kudai nafasi yake kama mwanamume, hususan katika jamii ya Waswahili kwa sababu ametekeleza wajibu wake wa kukidhi jamii kama mwanamume. Asingepata tunuku la hadhi ya mwanamume pasipo kutimiza jukumu hili. Maoni ya Bliss (1974) na Marwel (1975) yanabainisha kuwa mwanamume anapokosa kutekeleza jukumu lake la kukimu familia anakuwa na hofu ya kupoteza hadhi yake katika jamii. Wanadokeza kuwa kwa sasa jukumu la kukimu familia lililotengwa kwa mwanamume limeingiliwa na mwanamke na kusababisha hali ya kutishia nafasi ya mwanamume ya kuwa 'mkimu familia' na 'mfalme wa kasri'. Wahojiwa (Sudi, Zhura, Kefa, Salim, Bakari, Hama, Obo, Suleiman, Mponda, Vae, Abdalla, Haji, Amina, Mwanahawa na Nabhany wa Tana River na Lamu) walidokeza kuwa nafasi na majukumu aliyotengewa mwanamume katika jamii ya Waswahili kwa misingi ya itikadi, mila na desturi imevurugwa kutokana na elimu na mabadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Mabadiliko haya yamezua mgogoro wa mahusiano baina ya mwanamume na mwanamke miongoni mwa Waswahili.

Baadhi ya wanaume katika jamii ya Waswahili walionesha mtazamo wa kuafiki mabadiliko yanayolenga jinsi ya kiume. Mhojiwa Sudi wa Tana River, alibainisha kwamba wanawake wa jamii ya Waswahili sasa hutekeleza majukumu ambayo awali yalitengwa kwa ajili ya jinsi ya kiume. Wahojiwa Suleiman na Swale wa Tana River wanaona kuwa majukumu ya kifamilia yanapaswa kutekelezwa kwa ushirikiano baina ya mume na mke pasipo kuachwa kuwa mzigo kwa mwanamume pekee.

Mathalani, taswira anayopewa mwanamume katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kama mkidhia familia imezua mgogoro wa kimahusiano baina ya mwanamume na mwanamke. Hali ilivyo sasa ni kwamba, wanawake wa jamii ya Waswahili wameingia ulimwengu wa kiuchumi ambapo wanaajiriwa kazi na kuweza kuchangia katika jukumu la kukidhia familia. Mwanamume si tegemeo la pekee katika kukidhi familia na jamii. Hali hii imekuwa tishio kwa hadhi na utukufu aliopewa mwanamume kwa misingi ya jukumu na nafasi aliyotengewa kama 'mkidhia jamii' na 'mfalme wa kasri' katika jamii ya Waswahili. Haya ni kutokana na *Utenzi wa Fumo Liyongo* pamoja na mhimili wa nadharia ya Ubabedume inayoongoza utafiti huu kulingana na Bliss (1974), Peplan (1983) na Marwel (1975).

Kulingana na utafiti wetu mjini Lamu na maoni tuliyopata kutokana na kushuhudia mahakama ya kadhi, matarajio ni kwamba mume lazima akidhi mahitaji ya familia yake kikamilifu hata kama hana ajira. Maoni haya yameendelezwa pia na mhojiwa Nabhany wa 'Swahili Cultural Centre' ambaye alisema kuwa ni jukumu la mwanamume kukidhi kila hitaji la familia yake bila kumhusisha mkewe hata ikiwa mke ana ajira. Mtazamo huu ndio uliowaelekeza baadhi ya wanawake tuliowashuhudia katika mahakama ya kadhi kutaka talaka kwa madai kwamba waume zao hawakutekeleza jukumu la kuwalisha na kuwavisha, kulingana na mila na itikadi za Waswahili.

Mtazamo wa baadhi ya wanaume katika jamii ya Waswahili kuhusu ubabe na urijali umebadilika. Mhojiwa Swale wa Tana River ana maoni kuwa ubabe hauna maana katika mazingira ya sasa iwapo hauambatani na elimu, kazi na uwezo wa kiuchumi. Mhojiwa Zhura wa Tana River ameshadidia mtazamo huu anaposema kuwa hakuona haja ya mwanamume kuwa na urijali bila uwezo wa kiuchumi na kukimu jamii. Mwamko wa wanaume ni ishara kwamba wanaume wameitafakari upya hali yao katika jamii ambapo wamo mbioni kujikomboa kutokana na mifumo ya kitamaduni ya jamii ya kiasili. Kama anavyodokeza Kobia (2008) na Doyle (1985), mabadiliko yataanza wakati ambapo wanaume kutoka kila sehemu na kiwango cha maisha pamoja na usuli wa kielimu wataanza kubadili mitazamo, tabia na imani yao. Imani hii huathiri siyo tu maisha yao bali maisha ya wale wanaowazingira pia.

**5.5 Mwanamume kama Msihiri**

Liyongo ana nguvu zisizo za kawaida ambazo zinatokana na usihiri. Hawezi kudhurika kwa njia yoyote ile, ila kwa kudungwa sindano ya shaba kitovuni. Asili ya nguvu zake ni siri na fumbo kwa watu kulingana na beti hizi:

143. Nisikiya wangu baba
liniuwalo ni haba
ni msumari wa shaba
kitovuni nkitiya

144. Jamii silaha piya
haziniuwi swabiya
ila nimezokwambiya
ni ya kweli yot'e piya

Siri ya nguvu za Liyongo inapogunduliwa kwa usaliti wa mwanawe, Liyongo anapoteza uwezo wake wa kujihami. Tukio hili limejumuishwa katika utenzi ili kukidhi vigezo vya utendi simulizi wa Kiafrika (Mulokozi, 1999:11), kwamba mhusika mkuu katika tenzi za Kiafrika ni shujaa ambaye alizingirwa na usihiri, ushirikina na nguvu za ajabu. Taswira anayopata Liyongo kutokana na kuwa na nguvu na maumbile yasiyo ya kawaida, imechangia sana kutukuzwa kwake katika jamii ya Waswahili. Kwa mujibu wa watafitiwa wetu (Salim, Obo na Bakari wa Tana River na Baddi wa Lamu) utukufu aliopewa Liyongo ulitokana na maumbile, urijali na ubabe wake ambao ulikuwa zaidi ya kiwango cha kawaida. Waswahili walimtambua kuwa 'mwanamume sahihi' ambaye walimtegemea kama mlinzi na mtetezi wao dhidi ya maadui. Walikiri kuwa Liyongo alikuwa mtu wa ajabu. Mhojiwa (Hama) wa Tana River anamtaja Liyongo kuwa nabii.

Dhana ya sehemu dhaifu katika mwili ambapo ndipo palipo na siri ya nguvu za shujaa, inapatikana katika fasihi ya mataifa mengine na jamii nyingine. Kwa mfano, ngano ya Luanda Magere wa jamii ya Waluo ambaye siri ya nguvu zake ilikuwa katika kivuli chake na ngano ya Sundiata ambaye nguvu zake zilitokana na ushirikina (Niane, 1965 :14). Pia, kuna Samsoni wa *Biblia* (Waamuzi 13: 16) ambaye nguvu zake zilikuwa katika nywele zake. Anaponyolewa tunaona akipoteza nguvu zake.

Hata hivyo, tunaporejelea nadharia ya ubabedume inayoongoza utafiti huu kwa kuzingatia tukio hili, tunapata kwamba Liyongo alikuwa na nguvu za ajabu na kutenda mambo ya ajabu ambayo huenda ni ya kiungu. Hali hii inaingiliana na nadharia ya ubabedume inayoongoza utafiti huu kutokana na maoni ya Prusak (1974) na Ruether (1974b) wanapoeleza kwamba mwanamume aliumbwa kwa mfano wa Mungu wa 'kiume'. Liyongo anabainika kuwa na uwezo wa kutenda mambo ya kiajabu yasiyo ya kawaida kama alivyo Mungu.

Kwa muhtasari, ubadedume umejitokeza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kuwa mwanamume ni shujaa, mbabe, rijali, mkidhia jamii na msihiri. Masuala haya yana misingi yake katika nadharia ya ubabedume.

**6.0 Hitimisho**

Sifa za ubabedume anazopewa mwanamume katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* zina misingi yake katika itikadi na tamaduni za jadi za jamii ya Waswahili. Wahojiwa katika wilaya ya Tana River walichangia katika kupambanua baadhi ya sifa anazopewa mwanamume katika *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Sifa hizi zimechukua mtazamo wa tamaduni za kijadi za jamii ya Waswahili. Mtazamo huu umezingatia nafasi na majukumu aliyotengewa mwanamume katika jamii ya Waswahili. Kulingana na nadharia ya ubabedume, imebainika kwamba wanaume wamelazimika kuchunguza upya nafasi na majukumu yao katika jamii kutokana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi katika ulimwengu wa sasa. Hata hivyo, changamoto ni namna ya kupanga upya na kufungamanisha vyema mahitaji ya wanaume pamoja na wanawake, bila kuzua mgogoro.

## Marejeo


Bliss, E.J. (1974) Plasma testrosterone: Correlation with aggressive behavior and social dominance in man. *Psychosomatic Medicine* 36, 469-475.

Chafetz, J. (1974). *Masculine / feminine or human*? Itasca, IL: Peacock Publishers.

Collins, R. (1971). A Conflict Theory of Sexual Stratification. In *Social Problems* 19,3-21.

Coward, R. and Ellis, J. (1977) *Language and Materialism*. London: Routhledge.

Cunningham, S. (1983). Women still do majority of childcare, housword APA *Monitor, November, 16*.

Fave, Della (1980). *The Meek Shall not inherit the Earth*: Self – Evaluation and the Legitimacy of Stratification. *American Social Review* 45: 955-071.

Doyle, J.A. (1985) Sex *and Gender.* Iowa: CW Brown Publishers.

Finnegan, R. (1970) *Oral Literature in Africa.*Nairobi: Oxford University Press.

Jeftha, A. (2006), The Construction of Masculinity and Risk-taking behaviour among adolescent Boys in seven schools in the Western Cape, University of Western Cape, (Not published).

Kijumwa, M. (1913). *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Dar es Salaam: IKR.

King'ei, K. (2001). Historical and Folkloric Elements in Fumo Liyongo's Epic, Folklore.Volume 16, 27th July 2007, http//haldsjas. Folklore. ee/ folklore.

Kimani, C. W. (2003). *Suala* la Dhuluma Dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu, Kenyatta (Haijachapishwa)

Kobia, J.M. (2008): Taswira za Kiuana katika Nyimbo za Tohara za Wanaume Miongoni mwa Waigembe. Tasnifu ya Uzamifu (PhD). Chuo Kikuu cha Kenyatta Nairobi. (Haijachapishwa)

Knappert, J. (1983). *Epic Poetry in Swahili and other African Languages*. Leideen: E.J. Brill.

Marwell, G. (1975). Why ascription: Parts of a more or less formal theory of the functions and dysfunctions of sex roles- *American Sociological Review*, 40, 445-455.

Mbele, J. (1997). The significance of Deception in the Liyongo Epic. *Kiswahili* Vol. 60: 7-14. Dar es Salaam: TUKI.

Momanyi, C. (2007). Partiarchal Symbolic Order: The Syllables of power as Accentuated in Waswahili. Poetry, *The Journal of Pan African Studies*, Vol. 1 no. 8.

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Chuo Kikuu cha Dar - es - Salaam:TUKI.

Nayak, A. na Kehily M.J. (2008). *Gender, Youth and Culture*: Young Masculinities and Feminities. New York: Palgrave Macmillan.

Niane, T. (1965). *Sundiata an Epic of The Old Mali*. London: Longman.

Okpewho, I. (1979). *The Epic in Africa: Towards a Poetics of the Oral Performance*. Univ. Press Columbia.

Peplan, L. (1983). Roles and Gender. In H. Kelly, et al. (Eds), Close Relationships (pp. 220 – 264). New York: W. H. Freeman.

Ruether, R. (1974b). *Religion and Sexism*, New York: Simon and Schuster.

Sokoloff, N. (1980). Between Money and Love. New York: Praeger.

Steer, E. (1870). *Swahili Tales as Told by Natives of Zanzibar*. Society for Promotion of Christian Knowledge, London.

Wells-Wilbon, R. na Holland, S (2001, December). Social learning theory and the Influence of male role models on African American children in PROJECT 2000. The Qualitative Report 6(4). (July 27th 2007), http://www.nova.edu/ssss/QR/QR6-4/wellswilbon.html.